

SHULE YA SEKONDARI AHMES

KISWAHILI KIDATO CHA PILI

KISWAHILI

KAZI YA LIKIZO DISEMBA

1. Taja dhima ya kila mofimu iliyopigiwa mstari:
 - i. Ukimwona mwambie aje.
 - ii. Wajumbe wamo mkutanoni.
 - iii. Watoto wote wameondoka.
 - iv. Amekufa
 - v. Jesca na Jongo walipendana sana
 - vi. Kilichopotea
 - vii. Kilichowasumbua
2. Tenganisha mofimu katika maneno yafuatayo:
 - i. Mgonjwa
 - ii. Sungura
 - iii. Waliompiga
 - iv. Karatasi
 - v. Mwanajeshi
3. Nini chanzo cha kuibuka kwa misimu?
 - i. Kwa nini watu hutumia misimu? Toa sababu sita za watu kutumia misimu.
 - ii. Onesha aina kuu za misimu.
 - iii. Misimu ina sifa pekee. Fafanua sifa bainifu sita za misimu katika lugha
 - iv. Taja huku ukieleza faida sita za kutumia misimu katika mawasiliano.
 - v. Matumizi ya misimu huleta athari kubwa katika lugha. Toa hasara sita za kutumia misimu.
4. Andika simu kwa Bwana Kasimu Luhende wa S.L.P. 355 Kamaka ukimweleza kuwa umefaulu kuingia kidato cha tatu. Jina lako liwe Atukuzwe Amani.
5. Elezea makosa ya kisarufi yanayojitokeza katika lugha
6. Eleza maana ya dhana zifuatazo za fasihi:
 - a) Taswira b) Uhakiki c) mtindo d) mapingiti e) taharuki f) kituo bahari g) mbazi h) mtazamo i) mizungu j) manju.
7. i. Kwa kutumia mifano ya kutosha jadili dhima nane za mofimu katika lugha.
 - ii. Fafanua kwa mifano dhima kuu sita za lugha kwa jamii.

- iii. Kwa kutoa mifano kwa kila hoja eleza maana ya nomino na fafanua aina sita za nomino.
 - iv. Mzungumzaji huongozwa na kanuni maalumu. Eleza mambo matano ambayo huwaongoza wazungumzaji.
8. Kwa kutunga sentensi moja kwa kila dhima, pigia mstari kiambishi “ki” kuonesha dhima zifuatazo:
- a) Kudunisha
 - b) Kuonesha ukaribu na msisitizo
 - c) Kuonesha sifa ya juu/ushujaa.
 - d) Kuonesha nafsi na njeo ya wakati ujao.
 - e) Kuonesha upatanishi wa kisarufi
 - f) Kuunda mzizi wa neno.
9. Jadili wahusika sita katika tamthiliya ya NGOSWE-PENZI KITOVI CHA UZEMBE.
10. Andika simu ya maneno kutokana na taarifa ifuatayo. Simu isizidi maneno kumi (10): Huruma Yatesha wa S.L.P.20 Mwanza amepata nafasi ya kazi Ileje, anatakiwa aripoti kabla ya tarehe 26-09-2021. Taarifa hii inatoka kwa Amani Mwema wa Ileje.